

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR  
BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR  
MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**102**

**KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2:30**

**IJUMAA 18 OKTOBA, 2024 MCHANA**

**MAELEKEZO KWA MTAHINIWA**

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MANNE (4) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu ya mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
12.		
JUMLA		
SAINI YA MHAKIKI		



0022476

**Mtihani huu una kurasa 13 zenye maandishi**

**SEHEMU A: (Alama 15)**

**UFAHAMU**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. Soma shairi hili kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.

Wapende baba na mama, Dunia uone njema, Usiachiwe lawama, Ili upate baraka,	upate zao baraka, uishi pasi na shaka, na mwisho kulaanika, heshimu baba na mama.
--	--

Wazazi wenye huruma, Uwape yao heshima, Ukiitwa nenda hima, Ili upate baraka,	kuwatukuza hakika, ili upate baraka, labeka kuwaitika, heshimu baba na mama.
--	---

Heshimu baba na mama, Baba umpe heshima, Ukigombana na mama, Ili upate baraka,	kiburi kukiepuka, naye mama kadhalika, laana takugubika, heshimu baba na mama.
---	---

Kumbuka baba na mama, Hivyo uwe na heshima, Kwa wazazi fanya wema, Ili upate baraka,	ni watukufu hakika, upate sitareheka, uweze kutakasika, heshimu baba na mama.
---	--

Heshimu baba na mama, Litadumu litavuma, Kukitokea zahama, Ili upate baraka,	ukitaka kutukuka, jina lako kusifika, wewe utasameheka, heshimu baba na mama.
---	--

Na yule aso na mama, Asidhani hana dhima, Walezi wape heshima, Ili upate baraka,	au baba katoweka, au amenusurika, kama wazazi hakika, heshimu baba na mama.
---	--

**Maswali**

- i. Andika jina la shairi hili.

---

---

- ii. Kwa kupitia ubeti wa tano, taja faida mbili (2) za kuwaheshimu baba na mama.

---

---

- iii. Taja mfano wa heshima ya kuwapa baba na mama.

---

---

- iv. Andika hasara mbili (2) za kugombana na wazazi.

---

---

- v. Kwa wale wasiokuwa na baba na mama wana dhima gani?

---

---

2. Fupisha ubeti wa pili wa shairi ulilosoma kwa sentensi isiyozidi maneno matano (5).

---

---

**SEHEMU B: (Alama 40)**

**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

**Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii.**

3. Tunga sentensi kwa kutumia miundo ifuatayo.

- i. N + V + T + E

---

- ii. W + t + N + V

---

iii. N + Ts + Ts + T

\_\_\_\_\_

iv. I + T + E

\_\_\_\_\_

v. T + E

\_\_\_\_\_

4. Tunga sentensi moja (1) kwa kila aina ya kiunganishi kifuatacho.

i. Kiunganishi chaguo

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

ii. Kiunganishi linganishi

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

iii. Kiunganishi nyongeza

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

iv. Kiunganishi sababu

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

v. Kiunganishi kihusishi

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

5. Andika maneno yenye maana sawa na maneno uliyopewa.

NA.	NENO	NENO LENYE MAANA SAWA
i.	Ndovu	
ii.	Sebule	
iii.	Mviringo	
iv.	Msalani	
v.	Wakati	

6. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi kwa kuzingatia alama za uandishi.

i. mama alipanda minazi miembe michungwa na migomba

---

---

ii. raisi anarudi leo kutoka pemba

---

---

iii. sisi ni wanafunzi hodari na walimu wanatupenda

---

---

iv. skuli zitafunga ijumaa

---

---

v. mwalimu mkuu anahutubia

---

---

7. Lugha ni kiungo muhimu katika jamii ya Kitanzania. Bainisha dhima tano (5) za Lugha za kijamii.

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

[illegible]**FASIHI**

8. Simulia hadithi fupi kwa maneno yasiyopungua mia moja (100) na yasiyozidi mia na hamsini (150) inayoendana na methali isemayo “MTAKA NYINGI NASABA HUPATA MWINGI MSIBA”.

[illegible]

This image shows a blank sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

9. Toa maana ya methali zifuatazo.

i. Haraka haraka haina baraka.

---

ii. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

---

iii. Mstahamilivu hula mbivu.

---

iv. Samaki mkunje angali mbichi.

---





---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

**SEHEMU D: (Alama 15)**

**UTUNGAJI**

**Jibu swali MOJA (1) katika sehemu hii.**

11. Andika Insha kwa maneno yasiyopungua mia na ishirini (120) na yasiyozidi mia na hamsini (150) kuhusu "ATHARI ZA DAWA ZA KULEVYA"

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

[illegible]

12. Andika barua kwa Mkurugenzi wa Viwanda na Masoko S.L.P 100 Zanzibar kwa ajili ya kuomba nafasi ya kazi ya Ukarani, anuani yako S.L.P 205 Mwembe Beni Zanzibar. Jina lako ni Siwajibu Majaliwa.

[illegible]

This image shows a blank sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.





